

Umri ya kufanya Makubaliano

Umri ya kufanya makubaliano ni umri ya chini yenye sheria inasema mutu anaweza sema “**ndiyo**” ku mambo ya kukuwa mu uhusiano ya kingono.

Haiko tu kuhusu kupenda kukuwa mu uhusiano ya kingono...



Sheria inasema kama vijana wenye wako na **umri** fulani habaya **komala**, habaya kuwa na **maarifa**, ao **kuelewa** mambo fulani kusudi bafanye ile uamuzi kwa usalama.

Sheria za umri ya kufanya makubaliano zimewekwa kwa kulinda watoto na vijana zidi ya unyonyaji na unyanyasaji. Kuvunja hizi sheria inaweza hesabiwa kuwa "ubakaji ya kisheria kwa mtoto" ao "makosa ya kingono," hata kama bote bawili balikubaliana.

Umri ya kufanya makubaliano ni gani mu inchi ya Marekani?

- Umri ya kufanya makubaliano inatofautiana kulingana na jimbo: inaweza kuwa miaka 16, 17, ao 18.
- Kama mutu iko na uhusiano ya kingono na mutu mwenye iko na miaka chini ya umri ya kufanya makubaliano, anaweza kushitakiwa kisheria hata -kama bote bawili balikubaliana.
- Majimbo fulani iko na sheria ya kipekee kama tofauti ya umri kati ya batu bawili ni ya kidogo (kwa mufano miaka 2 ao 3).
- Fungula hii viungo kwa kupata habari ya zaidi kuhusu [umri ya kufanya makubaliano](#) na sheria [za makubaliano](#) mu kila jimbo.

Juu ya nini umri ya kufanya makubaliano ni ya muhimu?

Kama mutu iko na uhusiano ya kingono na mutu mwenye iko na miaka chini ya umri ya kufanya makubaliano, anaweza kupata malipizi makubwa kwa ajili ya uhalifu, ikiwa amo kufungwa mu gereza na kuwekwa ku oroza rasmi ya baalifu ba [makosa ya kingono](#). Vizuwizi ingine inaweza kuwa, kama vile kutoruhusiwa kuishi karibu na masomo, mutu kutokuwa yeye peke na watoto, ao hata kuzuiwa kutumia intaneti.




Maelezo kuhusu hii kitabu inapatikana ku [WebMD](#), [WorldPopulation](#), na [RAINN](#).

Umri ya kufanya Makubaliano


Malipizi ya kuvunja sheria za umri ya kufanya makubaliano mu majimbo fulani:

California



Kulingana na tofauti ya umri, mushitakiwa anaweza kuhukumiwa kufungwa mu gereza na/ao kulipa **faini yenye inafikiya 25000\$ (Dola elfu makumi mbili na tano ya Marekani).**

Florida




Mukosaji anaweza kuhukumiwa mpaka **miaka 15** mu gereza na kulipa faini ya **10000\$ (Dola elfu kumi ya Marekani).**

New York



Kulingana na kosa yenye ilifanywa, mushitakiwa anaweza kuhukumiwa mpaka **miaka 25** mu gereza.

Texas



Kulingana na kosa yenye ilifanywa, malipizi inaweza kuwa kati ya miaka **2** mpaka miaka **99** mu gereza pamoya na faini yenye inafikiya **10000\$ (Dola elfu kumi ya Marekani).**

Ni nini inatokea kama mutu mukubwa iko na cheo ya uongozi?

Mu majimbo fulani, kwa kuzuwira matumizi ya mubaya ya mamulaka, hata kama mtoto ao kijana iko na umri yenye inaruhusiwa kisheria kufanya makubaliano, uhusiano inaweza kataliwa kisheria kama mutu mukubwa iko na cheo ya uongozi.

Hii inaweza kukuwa amo:

- Ba mwalimu ao bafanyakazi ba masomo
- Bafanyakazi ba kijamii
- Ba kocha ba michezo
- Maafisa wa vituo ya kufunga batu
- Bafanyakazi ba afya



Unaweza kufanya nini?

1. [Jifunze sheria zenye zinatumiwa mu jimbo yako.](#)
2. [Zungumuza na mutu muzima mwenye anaaminika.](#)
3. [Kumbuka kama usalama na ustawi yako njo ya muhimu zaidi](#)

Maelezo kuhusu hii kitabu inapatikana ku [WebMD](#), [WorldPopulation](#), na [RAINN](#).